JLLE
Vol 18(2) 1–24
© The Publisher
DOI:10.56279/jlle.v18i2.1

# Changamoto za Wanafunzi Wanaojifunza Lugha ya Kichina kama Somo kwa Wajifunzaji Wanaotumia Kiswahili Kama Lugha ya Kwanza katika Kumudu Stadi za Lugha: Mifano kutoka Shule Teule za Sekondari Nchini Tanzania

*Rabiel Shabani Fadhili*[1]

**Ikisiri**
*Kichina ni lugha mojawapo kati ya lugha za kigeni zinazofundishwa katika shule za sekondari nchini Tanzania. Katika kuboresha zoezi zima la ujifunzaji na ufundishaji wa somo la kichina katika shule za sekondari, makala hii imelenga kubainisha changamoto zinazokwamisha wanafunzi kuwa mahiri na namna bora ya kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Utafiti huu uliwahusisha walimu na wajifunzaji katika shule za sekondari zinazofundisha kichina katika mkoa wa Dodoma, halmashauri ya jiji la Dodoma. Shule ya sekondari Umonga, Dodoma na Kiwanja cha Ndege zilihusishwa katika utafiti huu. Aidha, mbinu za mahojiano, uchambuzi matini na ushuhudiaji zilitumika kupata data za utafiti huu. Mkabala wa kitaamuli uliongoza uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwasaidia watunga sera na wadau mbalimbali wa elimu, kuongoza uboreshaji wa ufundishaji wa lugha na utoaji wa rasilimali. Kimsingi matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa zipo changamoto zinazokwamisha umahiri wa wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili kama vile; tofauti za kiisimu baina ya Kichina na Kiswahili, walimu kutokuwa mahiri katika lugha wanayofundisha, suala la mazingira finyu ya kujifunzia na upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Pia, utafiti huu utachangia katika mjadala mpana wa kitaaluma kuhusu elimu ya lugha za kigeni barani Afrika, na kupendekeza njia za uchunguzi wa siku zijazo.*

**Maneno Msingi:** *Lugha ya pili, Kichina, Kiswahili, lugha za kigeni*

**Abstract**
*Chinese is one of the foreign languages taught in secondary schools in Tanzania. In order to improve the overall learning and teaching process of Chinese in secondary schools, this article identifies the challenges that*

[1] **Coresponding Author:**
Assistant Lecturer in Kiswahili Linguistics in the Department of Languages and Literature, Dar es Salaam University College of Education, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania. E-mail: rabielfadhili@gmail.com

*hinder students from becoming proficient in the language and suggests effective ways to address these challenges. The study involved teachers and learners in secondary schools in Dodoma City. The schools were Umonga, Dodoma and Kiwanja cha Ndege. Additionally, methods such as interview, text analysis, and observation were used in gathering data for this study. The analysis and presentation of data were guided by a qualitative approach. The findings of the study are expected to assist the policymakers and various educational stakeholders in improving language teaching and in resource provision. Essentially, the results indicate the several challenges that hinder the proficiency of leaners' studying Chinese as a second language from developing. Other challenges are teachers' lack of proficiency in the language, a limited learning environment, and a shortage of teaching and learning materials.*

**Keywords:** *Second language, Chinese, Kiswahili, foreign language*

## Utangulizi

Lugha ni kiungo muhimu sana katika elimu (Sardeshpande, 2020). Kiswahili na Kiingereza ni lugha za kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi ya kufundishia katika elimu ya awali na msingi hasa katika shule za umma, huku Kiingereza kikitumika kufundishia kwa shule zinazotumia mtaala wa Kiingereza hasa shule binafsi. Kwa upande wa elimu ya sekondari, Kiingereza ndiyo lugha ya kufundishia na kujifunzia huku Kiswahili kikibaki kama somo. Lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyinginezo za kigeni ikiwemo Kichina hufundishwa kama somo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo (MOE, 2014). Sera ya elimu na mafunzo nchini Tanzania inasisitiza juu ya umuhimu wa lugha za kigeni katika kuongeza ufahamu na umahiri katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Kichina ni moja ya lugha ya kigeni inayofundishwa katika shule za msingi na sekondari nchini Tanzania. Serikali ya Tanzania katika kusisitiza umuhimu wa lugha hiyo, mwaka 2015 iliandaa muhtasari wa kufundisha Kichina kwa shule za sekondari za awali. Kulingana na Bakari (2022) na Masanilo na Ammann (2024), lugha ya Kichina ilianza kufundishwa katika shule za sekondari mnamo mwaka 2016, ikianza na shule sita pekee na jumla ya wanafunzi 2631. Aidha, mpaka sasa zipo zaidi ya shule 25 za sekondari zinazofundisha lugha ya Kichina kama somo Tanzania nzima.

Pamoja na jitihada na mafanikio hayo ya serikali ya kuongeza idadi ya shule zinazofundisha somo la Kichina katika shule za sekondari, ambazo wajifunzaji wake hutumia Kiswahili kama lugha ya kwanza, bado zipo changamoto zinazowakabili wajifunzaji katika kumudu stadi za lugha. Aidha, tafiti zilizopo hazijaweza kushughulikia kikamilifu changamoto hizo na kufanya kuwa na pengo linalohitaji kushughulikiwa. Kimsingi, kuzielewa changamoto zinazowakabili wanafunzi wa shule za sekondari nchini Tanzania katika kumudu stadi za lugha ya Kichina ni muhimu kwa sababu kadhaa. Itawapa wadau wa elimu na walimu

taarifa muhimu kuhusiana na ufanisi wa mbinu za kufundishia na namna bora ya kuzitumia. Zaidi ya hayo, kujua changamoto ni hatua muhimu katika kuimarisha mfumo mzima wa elimu hasa katika ufundishaji wa lugha za kigeni kwa wajifunzaji ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza. Vilevile, makala hii itawasaidia wajifunzaji katika kuongeza umahiri wa lugha ya Kichina na hivyo kufungua milango ya fursa nyingi za kiuchumi na kijamii, ikiwemo kupata ufadhili wa kimasomo na fursa za ajira.

**Methodolojia**

Katika kupata data za utafiti huu, mbinu changamani zilitumika. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano, ushuhudiaji na uchambuzi matini. Ugwu na Eze (2023) wanaeleza kuwa, mahojiano ni mazungumzo ya ana kwa ana ambayo maswali yanaulizwa moja kwa moja kwa watoataarifa ili kutimiza lengo la utafiti. Katika mahojiano, mbinu ya mahojiano ya vikundi lengwa ilitumika. Kulingana na Ugwu na Eze (2023), mbinu ya mahojiano ya vikundi lengwa huzingatia kuhusisha idadi ya watu wanaohojiwa kwa wakati mmoja, ambapo mtafiti kwa kawaida huhimiza mwingiliano wa washiriki katika kikundi ili kupata uelewa wa mitazamo na mitazamo halisi kuhusiana na jambo linalotafitiwa. Mbinu hii huwafanya watoataarifa kuwa huru kujibu na kutoa maoni na mitazamo yao. Mbinu hii ilitusaidia zaidi kuelewa na kujifunza kuhusiana na tabia, mitazamo na maoni ya wajifunzaji kuhusiana na zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kichina wawapo shuleni na nyumbani. Vilevile, katika ushuhudiaji, mbinu ya ushuhudiaji asilia ilitumika, ambapo mtafiti hushuhudia matendo ya watoataarifa katika mazingira yao halisia (Ugwu na Eze, 2023). Mbinu hii ilitumika katika kupata uhalisia wa mazingira ya ndani na nje ya darasa kwa walimu na wajifunzaji.

Vilevile, mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika katika uteuzi wa eneo la utafiti ambapo mkoa wa Dodoma uliteuliwa kwani una shule zinazofundisha Kichina ambazo zipo karibukaribu na hivyo kumfanya mtafiti kupata data faafu kwa muda mfupi zaidi. Vilevile, shule zilizoteuliwa katika utafiti huu ziliteuliwa kilengefu kwani mkoa wa Dodoma una shule tatu pekee za sekondari zinazofundisha lugha ya Kichina na kwamba shule hizi zilikuwa faafu katika kutupatia data ya utafiti. Shule zote tatu ambazo ni; Kiwanja cha Ndege, Umonga na Dodoma zilihusishwa katika utafiti huu ili kupata data toshelevu, linganifu na wakilishi. Aidha, utafiti huu ulihusisha sampuli ya jumla ya watoataarifa 36; wanafunzi wakiwa 30 na walimu 6 kwa shule zote zilizoteuliwa katika utafiti huu ambapo mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kuwapata. Mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ilitumika kupata sampuli wakilishi kutoka katika kundi kubwa la wanafunzi kwani kila mwanafunzi alikuwa na nafasi sawa ya kuhusishwa katika utafiti huu. Kwa upande wa walimu, waliteuliwa kilengefu kwani kwa kila shule kulikuwa na walimu wawili pekee wa somo la kichina na hivyo kufanya idadi ya walimu 6 kwa shule zote tatu. Kwa kuzingatia mgawanyo sawa, katika kila shule walimu 2 na wanafunzi 10 walihusishwa.

Aidha, utafiti huu ulihusisha vitabu vya kiada vinavyotumiwa na walimu na wanafunzi katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji ili kutazama sarufi ya

lugha ya Kichina ambapo vitabu vya *Kuaile Hanyu I, II* na *III* vilihusishwa. Vilevile, mtafiti alihusisha madaftari ya wajifunzaji ili kuona makosa mbalimbali ya kiuandishi yanayofanywa na wajifunzaji. Matini nyingine iliyotumiwa na mtafiti ni muhtasari wa somo la kichina, toleo la 2015. Lengo la mtafiti kuhusisha muhtasari ni ili kuona mwongozo wa mbinu pendekezwa za kufundishia, vifaa pendekezwa na umahiri kusudiwa ambao mjifunzaji anapaswa kuupata baada ya kumaliza kujifunza ili kuhusianisha na uhalisia wake katika mazingira ya darasa. Hivyo, mbinu ya uchambuzi matini ilitumika ili kuelewa yaliyomo katika matini zinazotumika kufundishia na kujifunzia. Sambamba na hilo, mkabala wa kitaamuli uliongoza uchanganuzi wa data za utafiti huu ambapo mbinu ya uchanganuzi kimada ilitumika katika kupata, kutambua, na kufasiri data.

**Mkabala wa Kinadharia**

Utafiti uliongozwa na mawazo ya mkabala wa kimawasiliano ulioibuka kutokana na mawazo ya nadharia ya lugha kama chombo cha mawasiliano iliyoibuliwa na Hymes (1972). Hymes alisisitiza umahiri wa mawasiliano katika ujifunzaji wa lugha na kwamba lengo kuu la kujifunza lugha liwe ni kumfanya mjifunzaji kuwa mahiri katika mawasiliano. Kulingana na mkabala huu, lengo kuu la mwalimu liwe ni kuwawezesha wajifunzaji kuwasiliana kwa lugha lengwa. Ili kufanya hivyo, wajifunzaji wanahitaji kuwa na maarifa kuhusu miundo ya lugha, maana, na kazi zake. Wanahitaji kujua kwamba kuna miundo mbalimbali inayoweza kutumika kutekeleza kazi moja. Pia, muundo mmoja unaweza kutumika kwa kazi tofauti. Vilevile, wanapaswa kuwa na uwezo wa kuchagua muundo unaofaa zaidi, kulingana na muktadha wa kijamii na nafasi za wazungumzaji. Pia, wanapaswa kuwa na uwezo wa kudhibiti mchakato wa kujadili maana na wazungumzaji wenzao. Na hivyo, mkabala huu unasisitiza kwamba mawasiliano ni mchakato; maarifa ya miundo ya lugha pekee hayatoshi kumfanya mjifunzaji kuwa mahiri katika kuitumia lugha anayojifunza (Larsen-Freeman na Anderson, 2011)

Larsen-Freeman na Anderson (2011) wakimnukuu Littlewood (1981) wanazidi kufafanua kuwa, kazi ya mwalimu ni kuchochea mawasiliano darasani. Jukumu kubwa la mwalimu ni kuanzisha hali zinazoweza kuchochea mawasiliano. Wakati wa shughuli hizo, mwalimu anachukua nafasi ya mshauri, akijibu maswali ya wajifunzaji na kufuatilia utendaji wao. Anaweza kuandika makosa yao ili kuyashughulikia baadaye wakati wa shughuli zinazolenga usahihi zaidi. Wakati mwingine, anaweza kuwa 'mshiriki wa mawasiliano' akishiriki katika shughuli za mawasiliano pamoja na wanafunzi. Larsen-Freeman na Anderson (2011) wanasisitiza kwamba katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, wajifunzaji wanapaswa kuwa wasemaji zaidi. Hivyo, wajifunzaji ndio wenye wajibu zaidi katika kujifunza kwao na kwamba mwalimu anapaswa kuchochea utendaji kati ya wajifunzaji wenyewe.

Vilevile, mkabala huu unatoa mwanya wa matumizi ya lugha ya awali katika kujifunza lugha ya pili. Hata hivyo, inapowezekana, lugha lengwa inapaswa kutumika sio tu wakati wa shughuli za mawasiliano, bali pia hata wakati wa kuelezea shughuli kwa wajifunzaji au katika kutoa kazi za nyumbani.Wajifunzaji

wanatambua kwamba lugha lengwa ni chombo cha mawasiliano, sio tu kitu cha kusomwa. Hivyo, matumizi ya lugha ya awali ya mjifunzaji yanaruhusiwa lakini hayasisitizwi zaidi na kwamba yatakuwa yakipungua mpaka itafika wakati yatapotea kabisa.

Pia, mkabala huu unasisitiza zaidi wajifunzaji kuhusiana sana wao kwa wao. Wanapaswa kufanya hivyo kwa mipangilio mbalimbali: wawili wawili, watatu watatu, vikundi vidogo, na kundi lote.Vilevile, mkabala huu unatoa mkazo mkubwa kwenye kujifunza lugha ya pili katika mazingira halisi. Hii inajumuisha kutumia mbinu mbalimbali kama vile kufanya ziara za kielimu, kualika wageni darasani, kuwashirikisha wanafunzi na wazungumzaji asilia kama marafiki wa lugha, na kuishi na familia za wenyeji.

Kwa ujumla, mkabala huu ni muhimu na ulitufaa katika utafiti huu kwani unaonesha umuhimu wa kufundisha na kujifunza lugha kimawasiliano. Mkabala huu unasisitiza zaidi umahiri wa mjifunzaji katika stadi kuu za lugha ili kufanikisha dhima kuu ya lugha ambayo ni kuwezesha mawasiliano. Hivyo, makala hii imeainisha vipengele muhimu ambavyo kwa namna moja ama nyingine visipozingatiwa kama mkabala huu unavyosisitiza huweza kumfanya mjifunzaji asifikie katika umahiri wa juu wa kuweza kuitumia lugha katika mawasiliano yaani lugha ya Kichina. Aidha, mkabala huu ulituongoza katika kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia kuboresha zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili. Kwa msingi huo, mkabala huu ulikuwa faafu katika uchanganuzi data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu.

**Mapitio ya Maandiko**

Kipengele hiki kinafafanua maendeleo ya ufundishaji wa somo la Kichina nchini Tanzania. Aidha, maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti yalichambuliwa.

**Maendeleo ya Ufundishaji wa Somo la Kichina Nchini Tanzania**

Lugha ya Kichina ilianza kufundishwa katika shule za Sekondari nchini Tanzania mnamo mwaka 2016, ikianza na shule sita pekee za majaribio. Tokea kipindi hicho, idadi ya shule zinazofundisha somo hilo imeongezeka maradufu ambapo hadi kufikia mwaka 2023 takribani zaidi ya shule 25 za sekondari za serikali na binafsi zinafundisha Kichina. Wakati Kichina kinaanza kufundishwa hapa nchini, hapakuwepo na walimu wa Kichina wenye asili ya Tanzania na hivyo serikali iliwatumia walimu wazawa wa Kichina kufundisha katika shule zilizoteuliwa. Hata hivyo, ongezeko la idadi ya shule zilizokuwa zikifundisha somo la Kichina halikuendana na idadi ya walimu wazawa wa Kichina mashuleni, ambapo hadi kufikia mwaka 2019, shule kumi na sita zilikuwa tayari zimeanza kufundisha somo hilo na kufanikiwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya sekondari ya awali (Bakari, 2022; Masanilo na Ammann, 2024). Aidha, mwaka 2018 serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu na TAMISEMI[2] ilipata ufadhili kutoka serikali ya watu wa China kupitia jimbo la Henan kwa baadhi ya walimu wazawa wa

[2] Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

masomo ya lugha katika shule za sekondari kwenda nchini China katika Chuo Kikuu cha Aeronautics cha Zhengzhou, kupata mafunzo maalumu ya mwaka mmoja ya ufundishaji wa lugha ya Kichina ambapo lengo lilikuwa wamalizapo mafunzo yao warudi na kushirikiana na walimu wazawa wa Kichina kufundisha somo hilo. Mwaka 2019, kundi hilo la walimu lilifanikiwa kumaliza mafunzo yao na kurudi nchini. Mwaka 2020 uliibuka ugonjwa wa Virusi vya Korona (COVID-19) na hivyo kusababisha idadi kubwa ya walimu wa Kichina katika shule za sekondari kurudi China. Katika, muktadha huo, walimu wenye asili ya Tanzania waliopata mafunzo kwa mwaka mmoja nchini China walibaki wenyewe kufundisha somo la Kichina. Kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2020 mwezi Novemba, serikali iliajiri walimu wa kufundisha somo la Kichina waliohitimu katika vyuo vya ndani (TAMISEMI, 2020).

Vilevile, katika kuendeleza na kuikuza lugha ya Kichina hapa nchini, serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI ilitangaza kuanzisha tahasusi mpya mbili zilizokuwa na somo la Kichina ndani yake kwa shule za sekondari ya juu; KEC (Kiswahili, Kiingereza na Kichina) na KFC (Kiswahili, Kifaransa na Kichina). Shule mbili pekee ziliteuliwa kupokea wanafunzi waliokuwa wamekidhi vigezo vya kusoma tahasusi hizo ambazo ni Shule ya Sekondari Morogoro kwa wanafunzi wa kike na Shule ya Sekondari Usagara kwa wanafunzi wa kiume (TAMISEMI, 2021). Pia, katika kuwapa wanafunzi uwanja mpana wa kuchagua tahasusi, hivi karibuni serikali kupitia wizara ya elimu iliongeza idadi ya tahasusi ambazo zilijumuisha somo la Kichina (MOE, 2024). Katika hatua nyingine, serikali kupitia Wizara ya Elimu imefanya maboresho ya mtaala wa elimu ya msingi na sekondari. Katika maboresho hayo, somo la Kichina litaanza kufundishwa kuanzia elimu ya msingi. Aidha, kutokana na maboresho hayo, serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imekwishakuandaa muhtasari wa somo la Kichina kwa elimu ya msingi (TET, 2023).

Hata hivyo, pamoja na jitihada ambazo serikali na wadau mbalimbali wa lugha ya Kichina wamekuwa wakizifanya katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji bado zipo changamoto zinazowakabili wajifunzaji kufikia upeo wa juu wa umahiri katika lugha hiyo. Licha ya hayo, tafiti ambazo zimekwisha kufanyika kuhusiana na ufundishaji na ujifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili katika mazingira ya Tanzania zilijikita kuchunguza masuala mbalimbali kama vile, sababu zinazosukuma kujifunza Kichina kama lugha ya pili na hali ya mafunzo ya walimu wa Kichina kwa uchache (taz: Ilonga, 2018; Bakari, 2022). Pamoja na tafiti hizo, hakuna utafiti wa kina uliogusia suala la changamoto zinazowakumba wajifunzaji katika kumudu stadi za lugha na hivyo utafiti huu wa sasa ni muhimu katika kushughulikia pengo hilo la kimaarifa.

## Maandiko Yanayohusu Ufundishaji wa Kichina kama Lugha ya Pili na Ufundishaji wa Lugha kwa Ujumla wake

Sehemu hii inachambua maandiko muhimu kwa utafiti huu wa sasa ili kuonesha kilichofanyika tayari na mapungufu yaliyolazimu utafiti huu wa sasa kufanyika.

Hu (2010) alifanya utafiti ulioangazia vipengele vyenye ugumu kwa wanafunzi wanaojifunza Kichina kama lugha ya kigeni na kubainisha sababu zinazoleta ugumu katika vipengele husika. Data za utafiti wake zilikusanywa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Uingereza ambao Kiingereza ni lugha yao ya awali. Kwa njia ya usaili, mtafiti alibaini vipengele 34 vyenye ugumu kwa kuzingatia stadi kuu za lugha ; kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza. Katika vipengele hivyo vilivyobainika, sababu za ugumu wake zilionekana katika mambo makuu sita; sarufi, maneno, mapokezi ya kusikia, utendaji, matamshi na kumbukumbu. Utafiti wao umenufaisha utafiti wa sasa, kwani umefafanua vipengele vinavyoonekana kuwa na ugumu katika kujifunza Kichina kama lugha ya pili. Hata hivyo, utafiti wao unatofautiana na utafiti huu wa sasa kwani utafiti wao ulihusisha wanafunzi wa vyuo vikuu, huku utafiti wetu ukihusisha wanafunzi katika shule za sekondari. Vilevile, eneo la utafiti wao ni tofauti na eneo la utafiti wa sasa kwani utafiti wao ulifanyika Uingereza, eneo ambalo ni tofauti sana kiuchumi, kijamii na kisiasa na Tanzania.

Tofauti na Hu (2010), naye Obiakor (2020) alifanya utafiti unaohusu changamoto za kujifunza na kufundisha Kiingereza kama lugha ya pili katika shule za sekondari za Nigeria. Kwa ujumla, mtafiti alijikita kuchunguza mbinu zinazotumiwa na walimu, namna zinavyoweza kuwa changamoto kwa wajifunzaji kuwa mahiri katika kujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili. Pia, alitazama namna lugha mama inavyoweza kuwa kikwazo kwa mjifunzaji kuwa mahiri. Pamoja na hoja zingine, matokeo ya utafiti wake yalionesha kwamba upungufu wa walimu ni changamoto kubwa katika kufundisha na kujifunza Kiingereza kama lugha ya pili katika shule za sekondari nchini Nigeria. Aidha, mtafiti alipendekeza serikali inapoajiri walimu wa Kiingereza inapaswa kuwafanyia usaili kwanza ili kupima umahiri wao katika lugha kabla ya kuanza kazi. Kimsingi utafiti wa Obiakor (2020) ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwani umeonesha namna ambavyo mbinu za ufundishaji na umahiri wa walimu unavyoweza kuwa changamoto kwa wajifunzaji wa lugha ya pili hasa katika shule za sekondari. Hata hivyo, utafiti huu wa sasa ni tofauti na utafiti wao kwa sababu, utafiti wao ulijikita kutazama kipengele cha walimu na mbinu wanazotumia kufundishia na kujifunzia, huku utafiti wa sasa ukitazama changamoto zote zinazowakabili wajifunzaji ili kuwa mahiri katika Kichina. Vilevile, utafiti huu wa sasa unatazama changamoto zinazowakabili wajifunzaji wanaosoma Kichina kama lugha ya pili, Kiswahili kikiwa lugha yao ya awali, tofauti na utafiti wao unaotazama changamoto za kujifunza Kiingereza kama lugha ya pili ambapo lugha hizo mbili yaani Kichina na Kiingereza zikiwa na sifa tofauti kisarufi.

Kwa upande wa Chua na wenzake (2022), walifanya utafiti unaochunguza changamoto zinazowakabili wanafunzi wenye asili ya Malaysia katika kujifunza herufi za Kichina na mikakati ya kujifunzia. Kupitia uchanganuzi wa kimaelezo uliofanyika, mtafiti alibaini kuwa kuna ugumu kwa wanafunzi kusoma na kuandika herufi za Kichina. Vilevile, ilibainika kuwa suala la Kichina kuwa na herufi nyingi sana, namna nyingi za matamshi na stroku nyingi zinazotumika

kuandikia herufi za kichina ilikuwa ni changamoto kubwa kwa wanafunzi kuwa mahiri kwenye uandishi wa herufi za Kichina. Hivyo, kutokana na hali hiyo wanafunzi hutumia mbinu ya kukariri pekee katika kujifunza herufi za Kichina kiasi cha kuwafanya kutokuwa mahiri katika kuandika herufi za Kichina. Ingawa utafiti wao umetusaidia kuelewa sifa za herufi za Kichina lakini ni tofauti na utafiti huu wa sasa kwani utafiti wa sasa haujaangazia changamoto za uandishi wa herufi za Kichina pekee yaani stadi ya kuandika bali umedadavua changamoto zote zinazoweza kuwa kikwazo kwa wajifunzaji kuwa mahiri katika stadi zote za lugha ya Kichina. Vilevile, eneo la utafiti na sampuli iliyohusishwa katika utafiti wao, ni tofauti na utafiti wa sasa.

Vilevile, Azeem na wenzake (2022) walifanya utafiti uliokusudia kutoa muhtasari wa jumla wa ufundishaji wa lugha ya Kichina katika mfumo wa elimu wa Pakistani. Lengo mahususi la utafiti huo lilikuwa kubainisha masuala ya kinadharia na changamoto za kivitendo zinazokumba fani hiyo, na mwishowe kupendekeza suluhisho linalowezekana kwa matatizo hayo. Uchambuzi wa data zao unaonyesha kuwa elimu ya lugha ya Kichina nchini Pakistani inakabiliwa na changamoto kubwa katika maeneo mbalimbali kama vile; mtaala na nyenzo za kufundishia, mbinu za kufundishia na maendeleo ya kitaaluma ya walimu. Utafiti wao ulimsaidia mtafiti kuelewa changamoto anuwai zinazokabili zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kichina. Aidha, utafiti wao ulizingatia kuchanganua changamoto zinazokabili mfumo mzima wa elimu nchini Pakistani, tofauti na utafiti wa sasa uliokusudia kuchanganua changamoto zinazokabili ufundishaji na ujifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili katika elimu ya sekondari ya awali mahususi kwa wajifunzaji ambao Kiswahili ni lugha yao ya awali. Zaidi ya hilo, eneo lilioteuliwa katika utafiti wao lilikuwa tofauti kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kisiasa na utafiti huu wa sasa. Utafiti huu wa sasa ulifanyika nchini Tanzania. Hivyo, utafiti huu wa sasa ni muhimu sana katika kuboresha zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili nchini Tanzania.

Kwa ujumla, tafiti tangulizi hapo juu zinahusiana na utafiti huu wa sasa na zimekuwa mwongozo mzuri na faafu. Hii ni kwa sababu zimetusaidia kuelewa dhana ya lugha ya pili na ufundishaji wa lugha ya pili kwa ujumla wake. Aidha, tafiti hizo zimenufaisha utafiti huu wa sasa kwa kuonesha vipengele vinavyoonekana kuwa na ugumu katika kujifunza lugha ya pili. Hata hivyo, tafiti hizo tangulizi zimefanyika katika maeneo tofauti yenye hali tofauti za kisiasa, kiuchumi na kijamii ambapo utafiti huu wa sasa umefanyika nchini Tanzania. Vilevile, tafiti tangulizi zimenufaisha utafiti huu wa sasa katika kuelewa changamoto mahususi zinazowakumba wajifunzaji lugha ya pili, huku utafiti huu wa sasa ukijikita kuchunguza changamoto zote zinazowakumba wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili. Licha ya hayo, sampuli ya watoataarifa katika tafiti tangulizi kuhusiana na lugha zao za awali ilikuwa tofauti na utafiti wa sasa kwani sampuli ya watoataarifa wa utafiti huu wa sasa hutumia Kiswahili kama lugha ya awali. Kwa msingi huo, utafiti huu wa sasa ulilenga kushughulikia pengo la kimaarifa katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kichina kama lugha ya pili kwa

wazungumzaji ambao Kiswahili ni lugha yao ya awali mahususi katika changamoto zinazowakumba wajifunzaji.

**Changamoto Zinazowakumba Wajifunzaji wa Lugha ya Kichina Wanaotumia Kiswahili kama Lugha ya Kwanza**

Sehemu hii inabainisha kwa uwazi changamoto zinazowakumba wajifunzaji wa lugha ya Kichina katika kumudu stadi za lugha ambapo lugha yao ya awali ni Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa zipo changamoto changamani ambazo zinahusisha nyanja na wadau mbalimbali. Zipo changamoto zinazohusu wazazi, wajifunzaji wenyewe, walimu na mfumo wa elimu kwa ujumla wake na isimu ya lugha zinazohusika. Vipengele vifuatavyo vinafafanua hoja hizo kwa uwazi.

**Kutokuwapo kwa Usaidizi wa Vitendo Kutoka kwa Wazazi**

Wazazi wana nafasi kubwa katika kuimarisha stadi za lugha kwa wanafunzi wanaojifunza lugha za kigeni. Moja ya changamoto ambayo ilibainika baada ya kufanya mahojiano na wanafunzi, ni kutokuwapo kwa usaidizi wa vitendo kutoka kwa wazazi. Pamoja na kupata usaidizi wa karibu shuleni wazazi wana mchango mkubwa sana katika kumfanya mjifunzaji kumudu stadi za lugha hata kama wazazi hao hawajui kuandika na kusoma lugha ambayo watoto wao hujifunza. Motseke (2020) anafafanua kuwa, wazazi wana jukumu kubwa na muhimu katika ukuzaji wa lugha mama, na hivyo uzoefu na ujuzi huo wa lugha unaweza pia kutumika katika ukuzaji na uimarishaji wa stadi za lugha ngeni miongoni mwa watoto. Motseke anazidi kufafanua kuwa, lugha ya mama ikitumika sambasamba na lugha mpya anayojifunza mtoto huleta matokeo chanya katika kukuza stadi za lugha.

Vilevile, ilibainika kwamba wanafunzi wawapo nyumbani hawapati usaidizi wa vitendo katika kuimarisha stadi za lugha. Wazazi huliona somo la Kichina kama mzigo kwa watoto wao, na hivyo kuwahimiza kutoweka mkazo katika somo hilo na badala yake mkazo uwe katika masomo mengine ambayo kwa mtazamo wa wazazi huyaona ni masomo ya lazima. Maelezo yafuatayo yaliyonukuliwa kutoka kwa watoataarifa kwa kutumia mbinu ya mahojiano yanaonesha namna ambavyo wazazi hawatoi usaidizi wa vitendo na hivyo kuwakatisha tamaa wajifunzaji katika kumudu stadi za lugha.

> “*kwa mfano mimi nina ratiba ya kujisomea nyumbani, na somo la Kichina huwa ninajisomea siku ya jumapili usiku. Nikiwa nimekaa nasoma, mama ana tabia ya kuniita kila wakati, na ninapomjibu kwamba ninajisomea Kichina na kwamba aniache nimalize huwa ananijibu ‘wa kusoma Kichina utakuwa wewe, huna lolote, hebu njoo nikutume’”*
>
> **Chanzo:** Data ya Utafiti (2024)

Aidha, wazazi wengine huwakatisha tamaa watoto wao pale wanapotamka maneno ama sentensi za lugha ya Kichina, ambapo wengi wao huwatamkia maneno ya kuwakatisha tamaa, kwamba hawatakaa waweze kuimudu lugha hiyo. Wei (2011)

anashadadia kuwa, suala la wazazi kuwakatisha tamaa wajifunzaji katika mazingira ya nyumbani hudumaza kwa kiasi kikubwa ari na shauku ya wanafunzi kutaka kumudu stadi za lugha ya Kichina.

**Wanafunzi Kutolipa Uzito Unaostahili Somo la Kichina**

Katika makala hii tulibaini kuwa, wanafunzi waliowengi hawalipi uzito unaostahili somo la Kichina na hivyo kushindwa kumudu stadi za lugha. Wanafunzi wengi hawaelewi umuhimu wa somo hili katika hatua za mbele kitaaluma. Wanafunzi wanaanza kujifunza somo hili wakiwa na mtazamo hasi kwamba mara wafikapo kidato cha tatu wanaweza kuliacha somo hili. Aidha, wale wachache wanaoendelea kujifunza somo hili huona kwamba masomo ya ziada ikiwemo Kichina yapo mashuleni kama sehemu ya kupumzikia na kupotezea wakati na kwamba hayana mchango wowote kitaaluma mara wamalizapo elimu yao ya sekondari. Hivyo, wanafunzi waliowengi wanashindwa kumudu stadi za lugha ya Kichina kwani hawalipi uzito unaostahili somo hilo. Kujifunza lugha ya kigeni kwa kiasi kikubwa kunatokana na msukumo wa ndani ya mtu na hivyo msukumo wa nje huimarisha nia ya mjifunzaji kuendelea kujifunza na mwishowe kuwa mahiri katika lugha anayojifunza.

Ilonga (2018) anafafanua kwamba, hamasa ya mwanafunzi kutaka kujifunza lugha ya kigeni inaweza kutokana na mwanafunzi mwenyewe, mazingira yanayomzunguka na hata makundi rika. Ilonga anazidi kufafanua kuwa, wakati mwingine nia ya kutaka kuchangamana na jamii ya kigeni, kusoma nje ya nchi na hata kupata fursa za kazi ni baadhi tu ya sababu zinazowasukuma wanafunzi kujifunza lugha za kigeni. Hivyo, wajifunzaji kutokuwa na msukumo wa ndani na taarifa za awali kuhusiana na somo hili, huwafanya kushindwa kuweka mkazo zaidi katika kujifunza na matokeo yake kutokuwa mahiri katika lugha wanayojifunza. Vilevile, baadhi ya watoataarifa walionesha hali ya kutokujiamini na kuwa na mtazamo hasi kwa kuona ya kwamba hawana uwezo na hawatakuja kuweza kumudu kuongea kwa ufasaha lugha ya Kichina na hivyo kutolipa umuhimu unaostahili somo hilo.

**Upungufu wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia**

Vifaa vya kujifunzia na kufundishia vina athari kubwa ya kumfanya mjifunzaji aweze kumudu stadi za lugha. Katika makala hii tulibaini kuwapo kwa upungufu wa vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya wanafunzi na walimu. Kwa kiasi kikubwa walimu wamekuwa wakitegemea nakala tepe za mitandaoni. Aidha, nakala ngumu zilizopo hazitoshelezi mahitaji kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma somo la Kichina. Kwa mfano, shule ya sekondari Umonga ilikuwa na vitabu vya kiada hamsini na tano pekee kwa kidato cha kwanza chenye jumla ya wanafunzi mia mbili hamsini na tano. Vilevile, tulibaini kutokuwapo kwa vitendea kazi muhimu vya kufundishia somo la kichina ikiwa ni pamoja na kompyuta, spika na projekta. Kulingana na miongozo ya ufundishaji wa somo hilo ikiwa ni pamoja na muhtasari, huhitaji mwalimu kuwafundisha wanafunzi maneno mapya kwa kuwasikilizisha matamshi ya maneno hayo kutoka kwa wazungumzaji asilia wa

Kichina. Yaani, maneno hayo yawe yamerekodiwa kwa kutamkwa na mzungumzaji mzawa wa Kichina.

Pia, yapo mazoezi ng'amuzi yanayohitaji mjifunzaji kutazama picha na huku akisikiliza mazungumzo yanayofafanua picha husika, na kisha kubaini ikiwa ni mazungumzo sahihi ama si sahihi. Azeem na wenzake (2022) wanashadadia kwamba ufundishaji wa Kichina wenye tija na matokeo makubwa katika kumfanya mjifunzaji awe mahiri, vifaa vya teknolojia ya medianuwai vinaweza kutumika mwanzo hadi mwisho wa kipindi, iwe ni kuanzisha mada mpya au kufafanua maneno mapya, herufi za Kichina, sarufi, maandishi, au kuanzisha maarifa yanayohusiana na utamaduni. Kimsingi, vifaa hivyo saidizi vya kufundishia na kujifunzia husaidia kuimarisha stadi za lugha ya Kichina hasa stadi ya kusikiliza na kuzungumza.

Vilevile, Goldberg na wenzake (2003) wanaeleza kwamba, kompyuta zinaweza kutumika kuboresha ujuzi wa kuandika kupitia matumizi ya programu za ukaguzi wa tahajia na sarufi, pamoja na mawasiliano yasiyo rasmi na wanafunzi wengine kwa kutumia mazungumzo ya maandishi ya ana kwa ana katika mazingira ya kujifunza kwa kutumia kompyuta. Hivyo, ukosefu wa vifaa muhimu vya kujifunzia na kufundishia ni changamoto inayoathiri wanafunzi kumudu stadi za lugha kama sera ya elimu na mafunzo ya 2014 inavyotaka. Gross (1971) anaeleza kuwa, tendo la kujifunza haliwezi kukamilika ikiwa kuna uhaba wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Licha ya hayo, kupitia ushuhudiaji uliofanywa na mtafiti darasani, alibaini kuwa hata miundombinu ya madarasa si rafiki kutumia vifaa vya kiteknolojia kufundishia. Madarasa hayana miundombinu ya umeme inayowezesha kutumia vifaa kama kompyuta, projekta na spika.

**Suala la Mazingira Finyu ya Kujifunzia**

Utafiti huu umebaini kuwa, mazingira ya kujifunzia yana athari kubwa katika kuimarisha kiwango cha ujuzi wa stadi za lugha. Katika makala hii tulibaini suala la wanafunzi kuwa na mazingira finyu ya kujifunzia wawapo shuleni. Mazingira ya shule hayawapi nafasi wanafunzi kufanyia mazoezi kile walichofundishwa darasani wawapo nje ya darasa. Mazingira ya nje ya darasa hayawapi wanafunzi kukazia maarifa ya kile walichofundishwa darasani. Wanafunzi wanaeleza kwamba kumekuwa na kampeni nyingi zinazosisitiza juu ya umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kingereza na kwamba mwanafunzi atakapobainika anatumia lugha nyingine tofauti na Kiingereza atapata adhabu kali. Hivyo, wanafunzi hutumia ama huzungumza lugha ya Kichina wawapo darasani tu, tena wakati wa kipindi cha Kichina pekee. Pia, hata wale ambao hujaribu kuzungumza pindi wanapokuwa wenyewe bila mwalimu baadhi ya wanafunzi huwakashifu wale wanaojaribu kuweka jitihada za kufahamu lugha hiyo.

Vilevile, kwa kuwa Tanzania si jamiilugha asilia ya Kichina, wanafunzi wanakosa nafasi ya kuchangamana na wajifunzaji asilia wa lugha ya Kichina na kwamba hali hiyo hupunguza wigo wa wajifunzaji kutumia lugha ya Kichina hata wawapo ya nje ya shule. Pia, Wajifunzaji wanakiri kwamba, hakujawahi kuwa na mijadala na

makongamano yanayowakutanisha wanafunzi wanaosoma Kichina katika shule za Mkoa wa Dodoma hata nje ya mkoa. Hivyo, mazingira ya shule na nje ya shule hayawapi wanajifunzaji nafasi ya wao kuwa mahiri katika lugha ya wanayojifunza yaani Kichina.

**Suala la Tofauti za Kiisimu kati ya Kiswahili na Kichina**

Kipengele hiki kitafafanua tofauti za kiisimu kati ya Kiswahili na Kichina ambazo ni changamoto kwa wajifunzaji katika kumudu stadi za lugha. Ikumbukwe wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili wanatumia Kiswahili kama lugha yao ya awali. Hivyo, tofauti za kiisimu baina ya lugha hizi mbili haziwezi kuepukika kiasi cha kuwa changamoto kwa wajifunzaji.

***Changamoto za Kifonolojia***

Fonolojia ya lugha ya Kichina ni tofauti sana na fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Ni wazi kwamba kila lugha ina mfumo wake wa sauti, na mfumo wowote wa sauti una sifa zake zinazoitofautisha lugha moja na nyingine. Makala hii inagusia vipengele mbalimbali vya kifonolojia katika kubaini mzizi wa tatizo la wajifunzaji kushindwa kuwa mahiri katika stadi za lugha ya Kichina. Kimsingi, irabu za lugha ya Kichina kwa idadi ziko sita huku lugha ya Kiswahili ikiwa na irabu tano pekee. Hata hivyo Kichina kina ruwaza changamani ya irabu zake yaani irabu ambatani，tofauti na lugha ya Kiswahili. Jedwali Namba 1 na Namba 2 hapo chini hushadadia hoja hii kwa uwazi.

**Jedwali Na. 1: Irabu Msingi za Lugha ya Kichina**

| Na. | Irabu | Neno | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 01 | /a/ | 他（tā） | me |
| 02 | /o/ | 我（wǒ） | mimi |
| 03 | /e/ | 也（yě） | pia |
| 04 | /i/ | 你（nǐ） | wewe |
| 05 | /u/ | 去（qù） | kwenda |
| 06 | /ü/ | 女（nǚ） | msichana |

**Chanzo:** Odinye (2015)

**Jedwali Na. 2: Irabu Ambatani za Lugha ya Kichina**

| Na. | Irabu | Neno | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 01 | /ai/ | 白（bái） | eupe |
| 02 | /ei/ | 黑（hēi） | eusi |
| 03 | /ou/ | 口（kǒu） | mdomo |
| 04 | /ao/ | 好（hào） | vizuri |
| 05 | /iao/ | 小（xiǎo） | ndogo |
| 06 | /iou/（/iu/） | 有（yǒu） | kuwa na.. |
| 07 | /uai/ | 快 | haraka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | （kuài） | |
| 08 | /uei/（/ui/） | 贵（guì） | ghali |
| 09 | /ia/ | 家（jiā） | nyumba |
| 10 | /ie/ | 姐 (jiě) | dada mkubwa |
| 11 | /ua/ | 花 (huā) | ua |
| 12 | /uo/ | 国（guó） | taifa |
| 13 | /üe/ | 月（yuè） | mwezi |

**Chanzo:** Odinye (2015)

Kulingana na Massamba na wenzake (2001), irabu huainishwa kwa kutumia kigezo cha mwinuko wa ulimi, sehemu ya ulimi inayotumika kutamkia na hali ya midomo. Kwa mujibu wa Jedwali Namba 1 hapo juu, kwa kutumia kigezo cha mwinuko wa ulimi irabu za juu katika Kichina ni /i/, /u/ na /ü/, kati ni /e/ na /o/ na chini ni /a/. Vilevile, kwa kigezo cha sehemu ya ulimi tunapata irabu za mbele /i/ na /ü/, irabu ya kati /a/ na irabu za chini /e/, /u/ na /o/. Pia, kwa kigezo cha hali ya midomo tunapata irabu viringe /u/, /ü/ na /o/ na irabu si viringe /i/, /e/ na /a/. Aidha, tukirejelea Jedwali Namba 2 hapo juu, Kichina kina irabu ambatani 13 ambazo zimeanishwa kwa kigezo cha msikiko wa irabu ambapo tunapata irabu ambatani-mbele zenye msikiko wa juu 4 ambazo ni  ai, ei, ao na ou；irabu ambatani-kati zenye msikiko wa juu 4 ambazo ni iao, iou, uai na uei；irabu ambatani-nyuma zenye msikiko wa juu 5 ambazo ni /ia/, /ie/, /ua/, /uo/ na /üe/ (Mao, 2008；Odinye, 2015；Candra na Sukma, 2020). Ni vyema ikaeleweka kwamba, uambatani huo hauna athari katika utamkaji na kwamba irabu hizo hutamkwa mara moja kama fungu moja la sauti na hakuna kituo kati ya irabu moja na nyingine. Licha ya hayo, zipo irabu ambatani ambazo namna zinavyoandikwa na kutamkwa ni tofauti, mathalani tazama data namba 6 kwenye Jedwala Namba 2 inatamkwa /iou/ lakini huandikwa kama (iu) vilevile, data namba 8 inatamkwa /uei/ lakini huandikwa (ui). Zaidi ya hayo, Kichina kina Irabu ambatani nazali 16, ambazo zimeundwa na konsonanti nazali na irabu (Candra na Sukma, 2020). Hivyo, kutokana na uanishaji huo inaonekana ni namna gani wajifunzaji wa Kichina wanavyopata changamoto katika kumudu stadi ya kuzungumza kutokana na utofauti uliopo katika irabu za Kichina na Kiswahili.

Vilevile, zipo konsonanti ambazo zipo katika Kichina lakini katika Kiswahili hazipo na zingine zipo katika Kiswahili lakini katika Kichina hazipo, na hivyo kuleta changamoto kwa wajifunzaji kumudu stadi za lugha ya Kichina. Tazama Jedwali Namba 3 na Namba 4 hapo chini.

**Jedwali Na. 3: Konsonanti Ambazo Hazijibainishi katika Kiswahili**

| Na. | Kosonanti | Mfano wa Neno la Kichina | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 01 | /pʰ/ | 票(piào) | Tiketi |
| 02 | /ɕ/ | 谢谢（xiè xie） | asante |
| 03 | /ʈsʰ/ | 成绩（chéng jì） | matokeo |
| 04 | /ʈs/ | 真（zhēn） | sana |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 05 | /tʰ/ | 天气 (tiān qì) | hali ya hewa |
| 06 | /tɕʰ/ | 铅笔 (qiān bǐ) | penseli |
| 07 | /kʰ/ | 看书 (kàn shū) | kusoma (vitabu) |
| 08 | /tsʰ/ | 菜（cài） | mbogamboga |
| 09 | /ts/ | 昨天（zuó tiān） | Jana |
| 10 | /tɕ/ | 家具（jiā jù） | samani |
| 11 | /ʂ/ | 十（shí） | kumi |
| 12 | /ɻ/ | 肉（ròu） | nyama |

**Chanzo:** Data ya Utafiti (2024)

**Jedwali Na. 4: Konsonanti za Kiswahili Ambazo Hazijibainishi Katika Kichina**

| Na. | Konsonanti | Mfano wa neno la Kiswahili | Kichina |
|---|---|---|---|
| 01 | /g/ | gari | 汽车（qì chē） |
| 02 | /b/ | basi | 公车（gōng chē） |
| 03 | /ʧ/ | chumba | 房间（fáng jiān） |
| 04 | /d/ | dawa | 药 (yào) |
| 05 | /ʤ/ | joto | 热（rè） |
| 06 | /ɣ/ | ghala | 库房（kù fáng） |
| 07 | /ʃ/ | shati | 衬衫(chèn shān) |
| 08 | /v/ | vaa | 穿(chuān) |
| 09 | /z/ | zabibu | 葡萄(pú tao) |
| 10 | /j/ | yai | 蛋(dàn) |
| 11 | /w/ | wali | 米饭（mǐ fàn） |
| 13 | /ɲ/ | kuangalia | 看看(kàn kan) |
| 14 | /ŋ/ | nyekundu | 红 (hóng) |
| 15 | /r/ | robo (saa) | 刻(kè) |
| 16 | /t/ | taifa | 国（guó） |

**Chanzo:** Data ya Utafiti (2024)

Katika kuchunguza Jedwali Namba 3 na Namba 4 hapo juu, inaonesha ni namna gani utofauti katika sauti za konsonanti kati ya lugha hizo huwa ni moja ya changamoto kwa wajifunzaji kwani wajifunzaji kwa upande mmoja huhamisha maarifa ya lugha ya kiswahili kujifunza lugha ya Kichina na kwamba wajifunzaji wengi hutamka konsonanti za Kichina kama wanavyotamka konsonanti za kiswahili. Jambo, hili lilijibainisha wazi wakati mtafiti anafanya ushuhudiaji darasani na kugundua changamoto hiyo kwa wajifunzaji katika kutamka konsonanti za Kichina. Aidha, kupitia mbinu ya mahojiano, wajifunzaji walionesha ugumu katika kutamka konsonati sahihi, yaani matamshi yao yalionekana kuathiriwa zaidi na kiswahili.

Licha ya hayo, Kichina ni lugha ya toni, yaani ni lugha ambayo mabadiliko ya toni katika sauti yanaweza kutumika kubainisha tofauti katika maana ya maneno. Kulingana na Sun (2006) Kichina kina toni aina tano. Tazama Jedwali Namba 5 hapo chini.

**Jedwali Na. 5: Toni za Lugha ya Kichina**

| **Toni** | **Kidatu cha Toni** | **Thamani ya Kidatu** | **Neno la Kichina** | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| Toni ya 1 | Toni ya juu | 55 | 妈 (mā) | mama |
| Toni ya 2 | Toni ya juu ya kupanda | 35 | 麻 (má) | aina ya mmea |
| Toni ya 3 | Toni ya shuka-panda | 214 | 马(mǎ) | farasi |
| Toni ya 4 | Toni ya kushuka | 51 | 骂(mà) | kukemea |
| Toni ya 5 | Toni isiyo na upande (neutral) | | 吗(ma) | kipashio cha uliza ( ?) |

**Chanzo:** Odinye (2015)


Kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 5 hapo juu, toni huwekwa katika irabu, aidha kila toni inapobadilika na maana ya neno hubadilika. Hali hii ni tofauti katika Kiswahili kwani mabadiliko ya maana ya maneno yake hayazingatii toni. Katika kujifunza lugha ya Kichina toni ni kipengele cha msingi sana kwa mjifunzaji kukielewa, ambapo kushindwa kukielewa ni sawa na kukanganya taarifa na mawasiliano kwa ujumla wake. Katika makala hii tulibaini wajifunzaji wengi hawamudu kutamka silabi ama maneno kwa kuzingatia toni sahihi, na kwamba utofauti huu baina ya lugha hizi mbili ni changamoto kwa wajifunzaji katika kumudu stadi ya kuzungumza na hivyo kukwamisha mawasiliano.

### *Changamoto za Kiothografia*

Kichina ni lugha inayotumia herufi maalumu kuandikia maneno yake. Herufi za lugha ya Kichina zina mfumo na sheria za kiuandishi ambazo wajifunzaji wanapaswa kuzifuata. Hivyo, uandishi wa maneno ya lugha ya Kichina unafuata kanuni zinazowesheza kuandika kwa usahihi. Katika kuandika, stroku maalumu zinaunganishwa kwa kufuata kanuni maalumu ili kupata herufi za Kichina. Zipo stroku msingi na stroku ambatani, ambapo stroku ambatani hutokana na stroku msingi. Jedwali Namba 6 hapo chini linashadadia hoja hii.

**Jedwali Na. 6: Stroku Msingi za Lugha ya Kichina**




| **Na.** | **Stroku Msingi** | **jina** | **Mfano** | **Inavyoandikwa** |
|---|---|---|---|---|
| 01 |  | 横 (héng) → | 一（yī）（moja） | Ni stroku ya ulalo inayoandikwa kutokea kushoto kuelekea kulia |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 02 |  | 竖(shù) ↓ | 十（shí）(kumi) | Ni stroku ya wima inayoandikwa kutokea juu kuelekea chini |
| 03 |  | 撇 (piě) ↙ | 力（lì）(nguvu) | Ni stroku ya kushoto-mdondoko inayoandikwa kutokea juu kuelekea chini kushoto |
| 04 |  | 捺(nà) ↘ | 八（bā）(nane) | Ni stroku ya kulia-mdondoko ambayo huandikwa kutokea juu kuelekea chini kulia |
| 05 |  | 点(diǎn) ↘ | 们（men）(kipashio cha wingi katika viwakilishi na nomino zinazotaja watu) | Ni doti inayoandikwa kutokea juu kwenda chini kulia |
| 06 |  | 提(tí) ↗ | 我（wǒ）（mimi） | Ni stroku ya kuelekea juu ambayo huandikwa kutokea chini kushoto kwenda juu kulia |

**Chanzo:** Xun (2010)

Jedwali Namba 6 hapo juu, huonesha stroku msingi za lugha ya Kichina na namna zinavyoandikwa. Aidha, kupitia stroku msingi tunapata stroku ambatani kama vile, 横钩 (hénggōu ⤵), 竖钩 (shùgōu ), 弯钩 (wān gōu ),斜钩(xiégōu ),卧钩 (wògōu ), 竖折 (shù zhé ) na 撇点(piě diǎn) kwa uchache. Zaidi ya hayo, zipo sheria ambazo zinapaswa kufuatwa katika kuzipangilia stroku wakati wa kuandika herufi za Kichina. Tazama Jedwali Namba 7 hapo chini.

**Jedwali Na. 7: Sheria ya Kupangilia Stroku**


| Mfano | Mpangilio wa Stroku | Sheria ya Kuandika |
|---|---|---|
| 十 |  | Stroku ya ulalo kwanza ndipo ifuate stroku ya wima |
| 人 |  | Stroku ya kushoto-mdondoko huanzwa kuandikwa kabla ya stroku ya kulia-mdondoko |
| 好 |  | Maliza stroku za kushoto kwanza ndipo uanze za upande wa kulia |
| 只 |  | Maliza stroku za upande wa juu kwanza ndipo uanze stroku za upande wa chini |

| | | |
|---|---|---|
| 月 |  | Zinapaswa kuanzwa stroku za nje ndipo zimaliziwe za ndani |
| 白 |  | Zimalizike stroku za nje kabla ya ndani, na ziandikwe za ndani kabla ya kufungwa |
| 小 |  | Katikati kwanza kabla ya pembeni |

**Chanzo:** Xun (2010)

Jedwali Namba 7 hapo juu, linaonesha sheria za kufuata katika kuzipangilia stroku wakati wa uandishi wa herufi za Kichina. Sheria zote hizi anapaswa kuzizingatia mjifunzaji wa lugha ya Kichina wakati anaandika herufi za Kichina. Pia, inapaswa ieleweke kwamba pinyini ni mfumo wa kiuandishi unaowasilisha taarifa za kifonetiki ambazo haziwezi kujibainisha katika herufi za Kichina. Hivyo basi, ili mjifunzaji aweze kumudu Kichina hasa katika stadi ya kusoma na kuandika anapaswa kuzijua herufi za Kichina vizuri kwani hakuna namna mjifunzaji ataweza kusoma vitabu na maandiko mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kichina. Kujifunza lugha ya Kichina kwa kutumia pinyini peke yake haitoshi kumfanya mjifunzaji kuwa mahiri zaidi sana ataambulia kuilewa stadi ya kuzungumza. Kwa mfano, unapotafuta herufi ya "wo" kwenye simu ama kamusi mtandao yoyote itakuwa ni vigumu kupata herufi kusudiwa kwani zitajitokeza herufi saba tofauti zinazorejelea pinyini hiyo moja. Vilevile, ni wazi kwamba Kiswahili kinafuata mfumo wa alfabeti kuandika maneno yake tofauti na ilivyo katika Kichina. Hivyo, kwa wajifunzaji wa Kichina wanaotumia Kiswahili kama lugha ya kwanza inakuwa changamoto kwao kumudu stadi ya kuandika maandishi ya Kichina. Tazama Kielelezo Namba 1, hapo chini kinachoonesha makosa ya kiuandishi kwa wajifunzaji.

**Kielelezo Na. 1: Makosa ya Kiuandishi**




**Chanzo:** Data ya Utafiti (2024)

Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonesha maneno ya Kichina ambayo hayajaandikwa kwa usahihi kutokana na wajifunzaji kutokufuata kanuni na taratibu za uunganishaji wa stroku zinazounda maneno ya Kichina.

Aidha, kupitia usaili uliofanyika baina ya mtafiti na wajifunzaji ulionesha namna ambavyo wingi wa sheria na kanuni za uandishi wa herufi za kichina unavyoweza kuwa kikwazo hasa katika kasi na usahihi wa maandishi wakati wa kuandika. Dondoo lifuatalo toka kwa watoataarifa linathibitisha hilo,

> *Kiukweli ninatumia muda mrefu sana wakati ninaandika maneno na sentensi za Kichina. Hii ni kwa sababu, sheria na kanuni za uandishi wa herufi za Kichina ni nyingi mno na hivyo kuniwia vigumu*


> *kuzishika na kuzifuata wakati wa kuandika. Pia, kushindwa kushika sheria hizo wakati wa kuandika, kunanifanya niandike herufi zisizo sahihi ama zenye makosa.*
>
> **Chanzo**: Data ya Utafiti (2024)

Hivyo, tofauti za kiothografia kati ya Kiswahili na Kichina ni changamoto inayosababisha wajifunzaji kushindwa kuwa mahiri hasa katika stadi ya kuandika.

**Suala la Lugha ya Kufundishia**

Lugha ya kufundishia ni nyenzo muhimu katika kuwafanya wajifunzaji waweze kupata maarifa mapana ya lugha wanayojifunza. Katika makala hii tulibaini kuwa, moja ya changamoto inayowakumba wajifunzaji katika kuwafanya wawe mahiri katika Kichina ni lugha inayotumiwa na walimu katika kufundishia. Katika usaili uliofanyika wajifunzaji walikiri kutokuelewa Kichina kwa sababu lugha inayotumiwa kuwafundishia ni changamoto kwao, yaani wajifunzaji hawana umahiri na lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha inayotumika kuwafundishia. Aidha, kupitia ushuhudiaji aliofanywa, mtafiti alijiridhisha kuwa walimu wanatumia lugha ya Kiingereza kufundishia dhana za Kichina. Katika kipengele cha kujifunza maneno mapya ya Kichina, mwalimu hutoa tafsiri ya maneno ya Kichina kwa lugha ya Kiingereza ambayo ni changamoto kwa wajifunzaji wengi. Vilevile, kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini, mtafiti alibaini vitabu vinavyotumika kufundishia lugha ya Kichina vimetumia Kiingereza kama lugha fafanuzi ya dhana za Kichina hasa katika kipengele cha maneno mapya. Kimsingi, suala la lugha ya kufundishia limebainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na mtaala na hivyo walimu hufuata miongozo hiyo. Suala hili linawafanya wajifunzaji kushindwa kuwa mahiri. Tazama Kielelezo Namba 2 hapo chini, kutoka katika kitabu cha kidato cha pili.

**Kielelezo Na. 2: Maneno Mapya ya Kichina Yenye Tafsiri ya Kiingereza**


**New Words**

1. 姓 (xìng) to be surnamed
2. 名字 (míngzi) name
3. 多 (duō) many, much
4. 朋友 (péngyou) friend
5. 谁 (shéi) who
6. 欢迎 (huānyíng) to welcome
7. 地方 (dìfang) place
8. 国家 (guójiā) country, nation
9. 号码 (hàomǎ) number
10. 你们 (nǐmen) you
11. 他们 (tāmen) they, them

**Chanzo**: Xiaoqi (2014)

Hivyo, Kielelezo Namba 2 hapo juu kinashadadia kwa uwazi changamoto ya lugha itumikayo katika kufafanua maneno ya Kichina. Kielelezo hicho kinaonesha maneno ya Kichina yenye tafsiri ya lugha ya Kiingereza.

**Suala la Upungufu wa Walimu Mahiri wa Lugha ya Kichina**
Mwalimu ni nyenzo muhimu katika kukamilisha zoezi la ujifunzaji. Umahiri wa mwalimu katika uwanja anaofundisha ni msingi wa kuwafanya wajifunzaji kupata maarifa faafu juu ya kile wanachojifunza. Mahojiano yaliyofanyika kati ya mtafiti na walimu wa lugha ya Kichina katika shule zilizoteuliwa ulionesha kuwa, walimu watatu pekee kati ya sita ndio waliofanikiwa kusoma Kichina kama somo la kufundishia walipokuwa vyuoni, huku walimu wawili wakiwa wamesoma kama kozi ya ziada. Aidha, mmoja kati yao alisoma Kichina kwa mwaka mmoja pekee kati ya miaka mitatu ya kusoma shahada ya awali. Katika mazingira hayo, ni vigumu baadhi ya walimu hao kuwa mahiri katika lugha ya Kichina, na hivyo kufanya wajifunzaji wa Kichina katika shule za sekondari kushindwa kumudu stadi za lugha hiyo. Mwalimu ni mwongozo na kioo kwa wajifunzaji, kushindwa kwake kutamka toni sahihi ama irabu ama konsonanti au hata kushindwa kuandika herufi za Kichina kwa usahihi hupelekea wajifunzaji kuakisi makosa ya mwalimu.

**Suala la Walimu Kutotumia Mbinu Shirikishi za Kufundishia**
Mbinu za kufundishia ni suala muhimu sana ambalo hurahisisha zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Ushuhudiaji uliofanywa darasani na mtafiti ulionesha namna ambavyo walimu hufundisha kinadharia zaidi na hivyo kuwafanya wanafunzi wasiwe mahiri katika utendaji. Zoezi la ufundishaji na ujifunzaji linapaswa kuwa shirikishi kati ya mwalimu na mjifunzaji, lakini katika makala hii tulibaini kuwa mwalimu ndiye mtendaji zaidi kuliko mjifunzaji. Kwa mfano wakati wa kujifunza muundo wa sentensi, mwalimu alikuwa akisoma sentensi huku wanafunzi wakimfuatisha na mwishoni huzitafsiri kwa lugha ya Kiingereza. Katika mazingira hayo wanafunzi wataishia kukariri tafsiri za mwalimu lakini hawatakuwa mahiri katika kuunda sentensi mpya na kuzitumia katika mawasiliano ya kawaida. Hivyo, mbinu zitumiwazo darasani na walimu hazimpi nafasi mjifunzaji kuwa mtendaji na hivyo kushindwa kuwa mahiri katika stadi za lugha anayojifunza

**Hitimisho**
Makala hii ilishughulikia changamoto zinazowakabili wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili katika kumudu stadi za lugha. Katika kupata data za utafiti huu, mbinu ya mahojiano, ushuhudiaji na uchambuzi matini zilitumiwa na mtafiti. Shule tatu katika mkoa wa Dodoma, halmashauri ya jiji la Dodoma zilihusishwa katika utafiti huu na jumla ya watoataarifa 36; walimu 6 na wajifunzaji 30 walihusishwa katika mgawanyo sawa. Vilevile, matini kama vile vitabu vya kiada, madaftari ya wajifunzaji na muhtasari wa somo la Kichina kwa shule za sekondari zilichambuliwa. Pia, mkabala wa kitaamuli uliongoza uchanganuzi wa data ya utafiti, ambapo mbinu ya uchanganuzi kimada imetumika. Vilevile, mawazo ya

kinadharia ya mkabala wa kimawasiliano yaliongoza uchanganuzi na uwasilishaji za data za utafiti huu.

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba zipo sababu mbalimbali zinazokwamisha wajifunzaji kuwa mahiri wa lugha ya kichina katika stadi zote za lugha. Imebainika kwamba, tofauti za kiisimu baina ya lugha ya awali ya mjifunzaji na lugha lengwa, hufanya wajifunzaji kuhamisha maarifa ya lugha za awali bila kuzingatia utofauti baina ya lugha hizo na hivyo kushindwa kuwa mahiri katika lugha wanayojifunza. Vilevile, matokeo yanaonesha kuwa, mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha lugha ya Kichina kama lugha ya pili hazimpi mjifunzaji nafasi ya kuwa mtendaji. Pia, mbinu zitumiwazo na walimu, hasa katika kujifunza maneno mapya ya Kichina zinamfanya mjifunzaji kukariri na si kumfanya mjifunzaji kuelewa mazingira ya utumiaji wa neno ama sentensi husika katika maisha ya kawaida. Sambamba na hayo, miundombinu ya darasa si rafiki katika utumizi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia, yaani madarasa yote yanayotumiwa katika zoezi zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kichina hayakuwa na umeme na miundombinu ya intaneti.

Licha ya hayo, imebainika kuwa, mazingira ya nje ya darasa hayampi nafasi mjifunzaji kutumia lugha katika mazingira halisi. Katika hilo, wajifunzaji walibainisha kwamba hakujawahi kuwa na makongamano na mijadala inayowakutanisha wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili na hivyo kushindwa kuimarisha uwezo wao wa kutumia lugha. Ni wazi kwamba lugha isipotumika ina kawaida ya kufa. Kwa upande mwingine, matokeo yanaonesha kwamba, wazazi kushindwa kujua umuhimu wa kujifunza Kichina kama lugha ya pili kumesababisha hali ya kuwakatisha tamaa watoto wao na hivyo kupunguza morali ya wajifunzaji kuijua lugha wanayojifunza. Wazazi wana mchango mkubwa katika kuimarisha stadi za lugha kwa wajifunzaji wa lugha ya pili, Kichina kikiwamo. Ili kuboresha zoezi zima la kufundisha na kujifunza Kichina kama lugha ya pili hasa katika kutatua changamoto zilizobainishwa katika makala hii, mtafiti anapendekeza mambo kadhaa.

Ipo haja ya walimu wanaofundisha Kichina kama lugha ya pili kujiimarisha katika mbinu zinazomjenga mjifunzaji kuwa mahiri katika kuitumia lugha katika mawasiliano. Mwalimu anapaswa kuwa mchocheaji wa hali zinazompa nafasi mjifunzaji kutenda zaidi. Makala hii inapendekeza walimu kutumia mbinu kama vile; utumizi wa nyimbo, michezo, uigizaji na utumizi wa vitu halisi katika kufundisha Kichina kama lugha ya pili. Sambamba na hilo, serikali inapaswa kuandaa mafunzo kazini kwa walimu wanaofundisha Kichina kama lugha ya pili ili kuimarisha ujuzi na stadi za kufundisha lugha hiyo. Mkakati huo wa mafunzo kazini utasaidia kuwakutanisha walimu katika shule mbalimbali zinazofundisha Kichina na hivyo kubadilishana uzoefu wa mbinu katika kufundisha lugha hiyo. Zaidi ya hayo, ili kuendelea kuimarisha ujuzi wa walimu katika lugha wanayofundisha ipo haja ya serikali kuwa na utaratibu wa mabadilishano ya walimu wa Kitanzania kwenda China na wanaotokea China kuja Tanzania. Hatua

hii itaboresha na kuimarisha zaidi ujuzi wa walimu kwani watapata nafasi ya kuchangamana na walimu wazawa wa lugha wanayoifundisha.

Aidha, makala hii inapendekeza serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa lugha ya Kichina, kuongeza vitabu mashuleni. Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania inahimizwa kuandaa vitabu vinavyozingatia lengo kuu la kujifunza lugha yaani mjifunzaji kuwa mahiri katika kutumia lugha anayojifunza. Vitabu hivyo viwe na kazi na mazoezi mengi yanayohimiza utendaji wa wajifunzaji. Sambamba na hilo, serikali inapaswa kuwekeza katika utoaji wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia vya kiteknolojia. Hatua, hii itaboresha na kurahisisha ufundishaji wa stadi mbalimbali za lugha kama vile, kusikia na kuzungumza kutoka kwa wamilisi wa lugha ya Kichina.

Vilevile, makala hii inapendekeza serikali kupitia Wizara ya Elimu na TAMISEMI kuboresha miundombinu inayotumiwa na wajifunzaji wa Kichina kama lugha ya pili hasa madarasa kuwekewa viunganishi vya umeme na intaneti. Hatua hii itawezesha walimu na wanafunzi kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile kompyuta, ubao janja, projekta na spika ambavyo kimsingi huhitaji umeme na inteneti ili viweze kutumika.

Pia, serikali na wadau mbalimbali wa lugha ya Kichina wanahimizwa kutoa elimu ya umuhimu wa kujifunza lugha hii kwa wanafunzi ili kuongeza morali ya wajifunzaji kujifunza lugha hiyo. Sambamba na hilo, ipo haja ya shule kuweka utaratibu wa kuanzisha idara itakayohusika na ushauri wa kitaaluma kwa wanafunzi. Pamoja na mambo mengine, idara hii itafanya kazi ya kutoa uelewa kwa wajifunzaji kuhusiana na umuhimu wa kusoma Kichina kama lugha ya pili na mwendelezo wake katika ngazi zingine za kitaaluma. Pia, elimu inahitajika kwa wazazi na walezi kuelewa kwamba lugha ya Kichina ina manufaa makubwa kwa watoto wao na kwamba wana nafasi kubwa ya kuimarisha na kuendeleza stadi ya lugha hiyo.

**Tamko la mgongano wa kimaslahi**
Mwandishi anatamka na kuthibitisha kutokuwapo kwa mgongano wa kimaslahi katika utafiti, uandishi wala uchapishaji wa makala hii

**Ufadhili**
Mwandishi anatamka na kuthibitisha kuwa hakupokea msaada wowote wa kifedha kutoka katika shirika ama taasisi yoyote ili kufanikisha utafiti wala uandishi wa makala hii

**Marejeleo**

Ammann, L. na Masanilo, D. S. (2024). Learning Mandarin Chinese in Tanzania : A Study of Tanzanian University Students. Katika J. Adeli & L. Ammann (Wah.), *New Silk Road Narratives: Local Perspectives on Chinese Presence along the Belt and Road Initiative*. Heidelberg: Heidelberg Asian Studies Publishing. Kur. 147-177.

Azeem, A., Naveed, T. na Jabbar, S. (2022). Chinese Language Teaching in Pakistan Problems and Solutions. *University of Wah Journal of Social Sciences*, 5(1): 55-80.

Bakari, M. M. (2022). A Study on Factors Influencing Chinese Language Learning in Tanzania. *IOSR Journal of Business and Management (IOSR-JBM)*, 24(2): 65-78.

Candra, H. na Sukma, Y. G. (2020). Comparative Analysis of Chinese and Indonesian Vowel Systems. *Humanus: Jurnal Ilmiah Ilmu-Ilmu Humaniora*, 19(1): 30-46.

Chua, H. W., Lee, H. L., Omar, S., Tohleheng, M. na Chin, S. M. (2022). Malaysian Non-native Chinese Students' Challenges and Learning Strategies in Chinese Characters Learning. *EDUCATUM Journal of Social Science (EJOSS)*, *8*(1): 67–82. https://doi.org/10.37134/ejoss.vol8.1.7.2022

Goldberg, A., Russell, M. na Cook, A. (2003). The Effect of Computers on Student Writing: A Meta-Analysis of Studies from 1992 to 2002. *Journal of Technology, Learning, and Assessment*, 2(1): 4-51. http://www.jtla.org.

Gross, N. (1971). *Implementing Organizational Innovation: A Sociological Analysis of Planned Education Changes*. New York: Basic Book Inc.

Hu, B. (2010). The Challenges of Chinese: A Preliminary Study of UK Learners' Perceptions of Difficulty. *Language Learning Journal*, 38(1): 99-118.

Hymes, D. (1972). On Communicative Competence. Katika J. Pride na J. Holmes (wah.). *Social Linguistics: Selected Readings*. Harmondsworth: Penguine Books. Kur. 269-293.

Ilonga, E. (2018). Motivation for Learning Chinese as a Foreign Language: Experiences from DUCE. *Journal of Education, Humanities and Sciences*, 7(2): 62-72.

Larsen-Freeman, D., na Anderson, M. (2011). *Techniques & Principles in Language Teaching*. New York: Oxford University Press.

Littlewood, W. (1981). *Communicative Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mao, S. Z. (2008). *Teaching Chinese Phonetic as a Foreign Language*. Shanghai: East China Normal University Electronic and Audio-Visual Press.

Massamba, D. P. B. & Wenzake. (2001). *Sarufi miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyuo* (Tol. 2). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Motseke, M. (2020). The Role of Parents in the Teaching of English First Additional Language in the Rural Area of Limpopo. *Per Linguam : A Journal of Language Learning = Per Linguam : Tydskrif Vir Taalaanleer*, 36(1): 112-124.

Obiakor, M. I. (2020). Problem of Teaching and Learning of English Language as a Second Language in Secondary Schools in Ankpa Local Government Area of Kogi State. *African Journal of Educational Management, Teaching and Entrepreneurship Studies*, 1(1): 76-88.

Odinye, S. I. (2015). Phonology of Mandarin Chinese: A Comparison of Pinyin and IPA. *Quarterly Journal of Chinese Studies; Xiamen University, China*, 4(2): 51-58.

Sardeshpande, M. (2020). Role of Language in Education. *Journal of Critical Reviews*, 7(8): 3852-3859.

Sun, C. (2006). *Chinese: A Linguistic Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

TAMISEMI. (2020). *Orodha ya Majina ya Walimu Waliopangwa Kwenye Vituo vya Kazi Novemba 2020*. TAMISEMI. https://www.tamisemi.go.tz/announcement/orodha-ya-majina-ya-walimu-waliopangwa-kwenye-vituo-vya-kazi-novemba-2020

TAMISEMI. (2021, Mar 29). *Utaratibu wa Kubadilisha Taasusi na Kozi za Vyuo kwa Kidato cha Nne 2020*. Youtube. https://www.youtube.com/watch?v=oaxH9YIkRys

Tanzania Institute of Education. (2015). *Chinese Language Syllabus for Ordinary Secondary Education: Form I - IV*. Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education.

TET. (2023). *Mtaala na Mihtasari ya Elimu Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). https://www.tie.go.tz/pages/draft-of-curriculum-and-syllabus-for-primary

Ugwu, C. N., na Eze, V. H. U. (2023). Qualitative Research. *IDOSR Journal of Computer and Applied Sciences*, 8(1): 20-35.

Xiaoqi, L. (2014). *Kuaile Hanyu: Student's Book II (Tol. 2)*. Beijing: Peoples Education Press.

Xun, L. (2010). *New Practical Chinese Reader Vol. 1 (Tol. 2)*. Beijing: Beijing Language and Culture University Press.

Wei, R. (2011). Parental Support for Chinese—English Bilingual Education: A Survey of Parents of Primary and Secondary Students in Shanghai. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 32(5), 481-496.

## Wasifu wa Mwandishi

**Bwana Rabiel Shabani Fadhili** ni Mhadhiri Msaidizi katika Isimu ya Lugha (Kitengo cha Kiswahili), Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Mwandishi anapendelea kufanya tafiti katika isimu tumizi, isimujamii, fonolojia, mofolojia na sintaksia. Kwa sasa mwandishi anafundisha kozi ya utangulizi wa misingi ya uandishi wa Kiswahili na sintaksia ya Kiswahili.